



قبر والوں کی 25 حکایات (Swahili)

VISA 25 ZA MAKABURINI

Sheikh-e-Tariqat, Amir-e-Ahl-e-Sunnat
Muasisi wa Dawat-e-Islami, Allamah Maulana Abu Bilal

MUHAMMAD ILYAS

Attar Qadiri Razavi

کاتب القرآن
القرآنی

قبر والوں کی 25 حِکایات

Qabr walon ki 25 Hikayaat

Visa 25 ZA MAKABURINI

Kitabu hiki kiliandikwa na Shaykh-e-Tariqat Amīr-e-Ahl-e-Sunnat, muanzilishi wa Dawat-e-Islami ‘Allāmah Maulānā Abu Bilal Muhammad Ilyas Attar Qadiri Razavi دامت بَرَکَاتُهُمُ الْعَالِيَةِ
Katika lugha ya Kiurdu. Kimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Majlise Tarajim. Endapo utaona makosa yoyote katika tafsiri yake au utungaji wake, tafadhali wasiliana na Majlise Tarajim kwa njia ya posta au kwa kipepesi ili upate thawabu.

Majlis-e-Tarājim (Dawat-e-Islami)

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagran,
Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan

UAN: ☎ +92-21-111-25-26-92 – Ext. 7213

Email: ✉ translation@dawateislami.net

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Dua Kabla Ya Kusoma Kitabu

Kabla ya kusoma kitabu au somo la kidini, soma dua ifuatayo.
Insha-Allah عَزَّوَجَلَّ utakumbuka yote uliyoyasoma.

اللَّهُمَّ افْتَحْ عَلَيْنَا حِكْمَتَكَ وَأَنْشُرْ
عَلَيْنَا رَحْمَتَكَ يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ

Ee mola عَزَّوَجَلَّ Ifungue milango ya elimu na busara kwa ajili yetu, na utuhurumie! Ewe ulie mtakatifu kabisa.

(Al-Mustatraf, vol. I, pp. 40, Dar-ul-Fikr, Beirut)

Kumbuka: Mswalie Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ mara moja kabla na baada ya dua.

Table of Contents

Dua Kabla Ya Kusoma Kitabu..... ii

Visa 25 ZA MAKABURINI 1

1. Adhabu Iliyoondolewa Kutoka Kwenye Makaburi Mia Tano Na Sitini (560).....	1
2. Makaburi yote Yalisamehewa Kwa Maombi ya Mcha Mungu... 2	
Misemo Mitatu ya Mtume ﷺ.....	4
Umar Alfaruq Alipozungumza Na Watu wa Makaburi.....	4
Ewe Binadamu Usiyejali! Matendo Mazuri Peke Yake Ndio Utaenda Nayo.	5
Jinsi ya Kutoa Salamu Makaburini.....	6
Kuweka Maua Kwenye Kaburi	7
Ni Nini Mtu Anapaswa Kutafakari Anapozuru Makaburi.....	8
3. Waridi au Nyoka	9
Wazikeni Waliokufa Karibu Na Watu Wema.....	10
4. Watu Wa Makaburini Walimjia Katika Ndoto.....	11
Roho Huja Majumbani Na Huomba Wafikishiwe Thawabu.....	12
5. Baraka Za Papo Hapo Za Kufikisha Thawabu	12
Tafsiri Ya Kumuona Mtu Aliyekufa Akiwa Mgonjwa Katika Ndoto	14
6. Alinikaribia na moto, na kama sio.....	15
Kwa Maombi Ya Walio Hai, Waliokufa Husamehewa,.....	15

7. Baba yake alimjia katika ndoto na akasema	15
9. Aliyoko Ndani Ya Kaburi Ni Kama Anayezama.	16
Ikiwa makaburi ya wazazi yako katikati ya makaburi, basi....	17
Kuhusu kukaa kando ya kaburi na kusoma Quran Tukufu	17
10. Vazi la Nuru	18
11. Sinia la Nuru	18
4. Maua Ya Madani ya KUTUMA THAWABU	19
Kaburi Likanawirika.....	19
Kitendo cha kuwafanya waliozikwa wote kua waombezi	19
Njia Ya Kupata Thawabu Idadi Ya Waliofariki	20
12-13. Ghaus-e-A'zam Sayiduna Sheykh 'Abdul Kadir Jaylani رحمته الله تعالى عَلَيْهِ alipozuru kaburi lilobarikiwa la Imam wake.....	21
10 maua ya madani kuhusu jinsi ya uzuru makaburi ya Mawalii.....	22
Durood-e-Ghausiyah	23
Kuzuru Makaburi ya Watu Wema ni Sunnah.....	24
Hupatikana Faida Kwa Kuzuru Makaburi Ya Mawalii.....	24
Usilibusu kaburi.....	24
Njia Ya Kutoa Salamu Katika Makaburi ya Mashahidi	24
Kuweka Tandiko Lenye Mapambo Juu Ya Kaburi	25
Kujenga Kuba juu ya Kaburi.....	25
Kuwasha Mataa Makaburini.....	26

Tawaf ya Kaburi.....	26
Kusujudia Kaburi.....	27
14. Kijana Aliyesoma Qurani Tukufu Ndani Kaburi	27
15. Kaburi Lenye Kunukia.....	28
16. Maiti Chongo	28
Kila Sahaba Wa Mtume Ni Mtu Wa Peponi.	29
17. Mfungwa Katika Kisima Cha Kiajabu	30
Hata Shahidi anayedaiwa madeni hataingia peponi mpaka.....	31
Kutoa Tangazo Kabla Ya Swala Ya Jeneza	32
18. Alifungua macho ndani ya kaburi.	32
Marafiki Wa Mwenyezi Mungu Wako Hai Hata Baada Ya Kufa.	33
19. Kwato Ya Ng’ombe Ilipokwama Kwenye Ardhi.....	33
20. Onyo Kwa Yule Aliyekaa Juu ya Kaburi.	34
21. Alipokanyaga Kaburi Alisikia Sauti.....	35
22. Mwenye Kaburi Alizungumza Na Mtu Aliyelala Juu Ya Kaburi.....	35
23. Inuka! Umeniudhi!	36
Kukanyaga Kaburi Ni Haramu.....	36
Ni Haramu Kutembea Kwenye Njia Iliyojengwa Kwa Kubomoa Makaburi.....	37
Ni Haram Kutembea Kwenye Sakafu Jirani Ya Makaburi Ambayo Imetengenezwa Kwa Kubomoa Makaburi.....	37
Kuweka uchafu karibu na kaburi	37
Ikiwa Mtu Anahitaji Kukanyaga Kaburi Wakati wa Kumzika Maiti Basi....?.....	38

Kuwalisha Vyakula Vitamu Chungu Makaburini.	38
Kunyunyiza Maji Kwenye Makaburi	39
Kuna Hukumu Gani Kujenga Nyumba Katika Makaburi ya Zamani?.....	40
Ikiwa Mifupa Imeonekana Katika Kaburi La Zamani...?.....	41
Hukumu ya Kufungua Kaburi Katika Misingi ya Ndoto.....	41
Watoto Kucheza Juu ya Kaburi	43
24. Aliyefukua Kaburi Akawa Kipofu.....	44
25. Mtu Aliyefukua Kaburi Alizikwa Akiwa Hai	44
Hukumu Ya Kuzika Kwa Muda Mfupi	45
Kuzika Bila Ruhusa Katika Kiwanja Cha Mtu.....	46
Kitu Gani Chatakiwa Kufanywa Ikiwa Mali Imezikwa Pamoja Na Maiti?.....	48

Maelezo 14 Kuhusu Kuzuru Makaburi.... 48

Jinsi ya Kutoa Salamu Makaburini.....	48
Dua Ya Kusababisha Kupata Maombi Ya Msamaha Kutoka Kwa Watu Mamilioni Waliofariki	49
Muda unaopendelewa kuzuru makaburi	50
Kufukiza Udi Juu Ya Kaburi	51
Kuweka Mshumaa Juu Ya Kaburi.....	51
Kaburi lisiloululikani kama ni la Muislamu au Asiyekua Muislamu.....	52

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Visa 25

ZA MAKABURINI

Bila hata kujali kiasi gani Ibilisi atajaribu kukupotosha, hakikisha umekisoma kijitabu hiki chote hadi mwisho;

إِنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ Imani yako itaimarishwa.



1. Adhabu Iliyoondolewa Kutoka Kwenye Makaburi Mia Tano Na Sitini (560)

‘Allamaah Abu ‘Abdullah Muhammad Bin Ahmad Maliki Qurtubi رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ amesimulia: ‘Mwanamke mmoja alimtembelea Sayiduna Hasan Basri رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ na akamuuliza, ‘Binti yangu mdogo amekufa. Tafadhali nifahamishe vipi nitaweza kumuona katika ndoto yangu.’ Alimuelezea la

kufanya. Kwa hivyo alimuona binti yake katika ndoto, hali ya kuwa amevishwa nguo za lami, alikua na minyororo shingoni mwake na miguu yake imefungwa kwa pingu. Kutokana na kuona sura hii ya kutisha, mama alianza kutetemeka.

Siku iliyofuata alimuelezea Sayyiduna Hasan Basri رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ ndoto hii, naye alisikita sana baada ya kuisikia. Baada ya mda mchache, Sayyiduna Hasan Basri رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alimuona msichana mmoja katika ndoto yake ambaye alikua amekaa juu ya kiti cha enzi na amepambwa taji juu ya kichwa chake. Msichana alipomuona, akasema, 'Mimi ndiye binti ya mwanamke aliyekuelezea hali yangu.' Sayyiduna Hasan Basri رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ akasema, 'Kulingana na vile alivyoieleza, ulikua unaadhibiwa عَذْرَاجَلْ Mabadiliko haya yalitokea vipi?' Marehemu msichana alijibu, 'Mtu mmoja alipita makaburini mwetu na akamsalia kipenzi Bwana Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Kutokana na baraka za sala ya Mtume, adhabu iliondolewa kutoka kwenye makaburi 560.' *(Imetolewa kutoka: Tazkirah fi Ahwaal-ul-Mauta-o-Umoor-il-Aakhirah, Juz.1, uk. 74)*

2. Makaburi yote Yalisamehewa Kwa Maombi ya Mcha Mungu

Wapenzi ndugu waislamu! Tumepata kujua kua sala ya Mtume ina Baraka kubwa na ikisomwa kwa ulimi wa mpenzi mkweli wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ, basi nguvu yake ni kubwa hata zaidi. Inawezekana kua aliyepita makaburini alikua mja

aliyependwa na Mwenyezi Mungu **عَزَّوَجَلَّ** na kwasababu ya kupita kwake makaburini na kumsalia Nabii, adhabu ya wenye makaburi 560 iliondolewa. Ni hakika kua ni faida kuwachukua wapenzi wakweli wa Mtume **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** kwa heshima kwenye makaburi ya jamaa zetu kuomba dua .

Baraka ya wacha mungu ni kubwa iliyoje. Siku moja Sayiduna Shaykh Ismail Hadrami **رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ** alipita makaburini, akasimama kando ya kaburi moja na akalia sana. Baada ya muda mfupi, alitabasamu kwa ghafla.

Alipoulizwa kuhusu jambo hilo alisema, ‘Niliona watu wa makaburi haya wakiadhibiwa, kwa hivyo nikaanza kulia na kuwaombea msamaha kwa Mwenyezi Mungu **عَزَّوَجَلَّ** kwa unyenyekevu. Hapo nikaambiwa, ‘Tumekubali uombezi wako kuhusu watu hawa.’ Baada ya kusema hivyo aliashiria kaburi ambalo lililokua pembeni na akasema, ‘Mwanamke ndani ya lile kaburi alisema, ‘Ewe Fakihi Ismail! Nilikua mwanamke muovu mwimbaji: Nami pia nimesamehewa?’ Nikamjibu ‘Ndiyo, wewe pia ni mmoja wa wale waliosamehewa.’ Hii ndiyo sababu ilyonifanya nitabasamu.’ *(Sharh-us-Sudoor, uk . 206)*

Mwenyezi mungu **عَزَّوَجَلَّ** awarehemu na atusamehe kwa baraka yao!

أَمِينَ بِجَاهِ النَّبِيِّ الْأَمِينِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Misemo Mitatu ya Mtume ﷺ

Tunatakiwa kuzuru makaburi ya waislamu, kwasababu hii ni Sunnah, ni njia ya kukumbuka akhera, ni njia ya msamaha wako mwenyewe na ni sababu ya faida kwa waliomo makaburini. Kulingana na hili, misemo tatu ya Mtume ﷺ imewasilishwa hapa chini:

- ❖ Niliwazuia kuzuru makaburi, lakini sasa zuruni kwani hili linaondoa mapenzi ya dunia, na linakumbusha Akhera. *(Sunan bin Majah, Juz. 2, Uk. 252, Hadithi 1571)*
- ❖ Mtu yeyote akipita kwenye kaburi la mtu ambaye alimfahamu duniani na akamtolea salam, basi maiti anamtambua na kumjibu salam yake. *(Tareekh-ul-Baghdad, Juz. 2, uk. 135, Hadithi 3175)*
- ❖ Yeyote atakayetebelea makaburi ya mzazi wake mmoja au wawili kila Ijumaa, atasamehewa na ataandikwa katika waja wema. *(Shu'ab-ul-Iman, juz. 6, uk. 201, Hadithi 7901)*

Umar Alfaruq Alipozungumza Na Watu wa Makaburi

Amir Al Muminina Sayiduna Umar AlFaruq رضى الله تعالى عنه siku moja alipita makaburini kisha akasema:

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا أَهْلَ الْقُبُورِ

(Amani iwe nanyi, enyi watu wa makaburini)

Habari mpya ni kua, wajane wenu wameolewa tena, watu wengine wanaishi kwenye nyumba zenu, na urathi wenu umesha gawanywa.’ Kisha sauti ilisikika, ‘Ewe Umar (رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ)! Habari zetu mpya ni kwamba tumepokea malipo ya matendo mema tuliyoatenda katika maisha yetu na tumepokea faida ya pesa tuliyoitumia kwa ajili ya mwenyezi mungu na tumepata hasara katika zile tulizoziacha ulimwenguni’ (*Sharh-us-Sudoor, uk. 209*)

Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ awarehemu na atusamehe bila hesabu kwa Baraka zao !



Ewe Binadamu Usiyejali! Matendo Mazuri Peke Yake Ndio Utaenda Nayo.

Wapenzi ndugu waislamu! Angalieni ukuu wa Amir al Muminina Sayiduna Umar Alfaruq (رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ)! Kwa uwezo aliyopewa na Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ alikua akizungumza na watu wa makaburi. Katika maelezo yaliyotajwa awali kuna mazingatio makubwa kwa wale ambao wana pupa ya mali na utajiri na wanaojenga majumba ya kifahari na kasri kubwa.

Ah! Nyumba ya kilimwengu ambayo mtu huijenga imara na huipamba vizuri, haibaki kwake milele. Hatimaye watu wengine wanairithi. Watu pia wanaumiliki utajiri wake na salio la benki alilojipatia kwa damu na jasho. Baada ya kifo, mali pekee itakayosaidia ni ile iliyotumiwa katika njia ya Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ. Katika Surah Ad-Dukhan, juzuu 25, aya 25-29 Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ amesema:

كَمْ تَرَكُوا مِنْ جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ ﴿٢٥﴾ وَزُرُوعٍ وَمَقَامٍ كَرِيمٍ ﴿٢٦﴾ وَنَعْمَةٍ كَانُوا فِيهَا فَاكِهِينَ ﴿٢٧﴾ كَذَلِكَ وَأَوْرَثْنَاهَا قَوْمًا آخَرِينَ ﴿٢٨﴾ فَمَا بَكَتْ عَلَيْهِمُ السَّمَاءُ وَالْأَرْضُ وَمَا كَانُوا مُنظَرِينَ ﴿٢٩﴾

Ni bustani ngapi na chemichemi waliziacha, na mimea na vyeo vitukufu, na neema walizokua wakistarehe nayo, Ndio hivyo! Na tukawarithisha haya watu wengine. La Mbingu wala ardhi hazikuwalilia wala hawakupewa muhula.

(Juzuu ya 25, Ad-Dukhan, Aya ya 25-29)

Jinsi ya Kutoa Salamu Makaburini

Wakati unapozuru makaburi, usimame namna ya kua uso wako umeelekea uso wa aliyezikwa na mgongo wako uelekee kibla. Kisha utoe salamu kama ilivyotajwa katika kitabu cha Tirmizi:

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا أَهْلَ الْقُبُورِ يَغْفِرُ اللَّهُ لَنَا وَلَكُمْ أَنْتُمْ سَلَفْنَا وَنَحْنُ بِالْآثَرِ

Tafsiri: Enyi watu wa kaburi, amani iwe nanyi, na Mwenyezi Mungu (عَدَّوَجَلَّ) atusamehe sisi sote. Nyinyi mmetangulia na sisi tutawafuata.’ (Sunan-ut-Tirmizi, juz. 2, Uk. 329, Hadithi 1055)



- ❖ Kuelezea hekima ya kutoa salamu kuelekea uso wa mwenye kaburi, Imam wa Ahli-Sunna, Imam Ahmad Raza Khan رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ amesema, ‘Unapozuru kaburi, uelekee uso wa mwenye kaburi na uje kwa upande wa miguu yake, ili uwe mbele yake apate kukuona. Usikaribie kaburi kutoka upande wa kichwa kwa kua hili litamfanya kuinua na kugeuza kichwa ili akutizame.

(Fatawa Razawiyyah, juz. 9, uk. 532)

- ❖ Lia zaidi na nyenyekea ukiomba msamaha kwa ajili yako mwenyewe na walioko makaburini. Kama huwezi kulia, basi angalau uwe na sura ya unyenyekevu.

Kuweka Maua Kwenye Kaburi

- ❖ Ni bora kuweka maua juu ya kaburi kwasababu mda wote maua haya yatakapobaki mazuri kwenye kaburi, yataendelea

kuleta tasbihi (kumsifu Mwenyezi Mungu **عَدَّوَجَلَّ**) na moyo wa aliyekufa utakaa ukifarajika. *(Rad-dul-Muhtar, juz. 3, uk. 184)*

❖ Pia hakuna ubaya ukiweka tandiko la Maua juu ya jeneza.

(Bahar-e-Shari'at, Juz. 1, Uk. 852)

❖ Nyasi mbichi na zenye unyevu zisiondolewe kutoka juu ya kaburi kwa kua rahma zateremka kutokana na tasbihi yake na aliyekufa anapata utulivu. Aidha, Kuondoa nyasi itakua kumnyima haki aliyekufa.

(Rad-dul-Muhtar, Juz 3, Uk.184)

Ni Nini Mtu Anapaswa Kutafakari Anapozuru Makaburi

Wakati unapozuru makaburi, badala ya kuzungumza kuhusu hili na lile na ubakie umezama katika fikra zisizo za maana, fanya Fikre Madina, yaani kumbuka kifo chako huku ukihesabu na ukitafakari matendo yako. Kumbuka dhambi zako, huku machozi yakimwagika machoni mwako, na ujiogopeshe kwa kufikiria adhabu ya kaburi. Tubu kwa Mwenyezi Mungu **عَدَّوَجَلَّ** na uzingatie moyoni kua, kama hawa watu waliokufa wako peke yao kaburini, si mbali mimi pia nitakua peke yangu nimeachwa katika kaburi lenye giza hali kadhalika. Vile vile kumbuka maneno ya hadithi yafuatayo, ﴿كَمَا تَدِينُ تُدَانُ﴾
Utavuna ulichopanda! (Al-Jami'-us-Sagheer, uk. 399, Hadithi 6411)

3. Waridi au Nyoka

Sayiduna Imam Sufian bin ‘Uyeyna رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ amesema:

عِنْدَ ذِكْرِ الصَّالِحِينَ تَنْزَلُ الرَّحْمَةُ

Rahma ya Mwenyezi Mungu hushuka wanapotajwa watu wema. (Hilyat-ul-Awliya, juz. 7, uk. 335, Hadithi 10750)

Wapenzi ndugu waislamu! Ikiwa hizi ni baraka za kuwataja watu wema, basi itakuaje kiwango cha rahma inayoshuka mahali ambapo watu wema wenyewe wapo. Bila shaka, waja wema wa Mwenyezi Mungu hudhihiri baraka zao ndani ya makaburi yao na waliozikwa karibu nao pia hufaidika na Baraka zao. Katika suala hili, imetajwa katika ukurasa wa 270 wa kitabu chenye kurasa 561 kitiwacho ‘*Malfuzaat-e-A’la Hadrat’*, kilichochapishwa na kitengo cha uchapishaji cha Dawat-e-Islami, Maktaba-tul-Madina: ‘Nilisikia Hadhrat Miyan Sahib رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ akisema kua, mahali fulani wakati mmoja kaburi lilifunguka na mwili wa maiti ulionekana. Kulikua na mitagaa miwili ya waridi yaliyouzunguka mwili wake na maua ya waridi mawili kwenye pua yake. Jamaa zake walidhania kua kaburi lilichimbika kutokana na uharibifu wa maji, wakachimba kaburi lingine sehemu nyengine na kuuweka mwili ule wa marehemu ndani. Sasa walipoangalia waliwaona nyoka wawili wakubwa wameuzunguka mwili na wanauuma uso wake kwa meno yao.

Watu walishangaa sana. Aliposimuliwa mtu mwenye busara alisema, ‘Nyoka wale wale walikuweco pale alipozika mwanzo pia (akimaanisha sehemu ya awali ya maziko), isipokua pale alikua karibu na kaburi la Walii wa Mwenyezi Mungu na kwa baraka yake, adhabu iligeuka kuwa rahma. Nyoka walionekana kua mitagaa ya waridi na meno yao kuoenaka kua maua ya waridi. Ikiwa mwamtakia uzuri huyu marehemu basi mregesheni pale na mumzike.’

Walipomregesha pale, mitagaa ile ile ya waridi ilionekana na pia maua yale yale ya waridi yalionekana.



Wazikeni Waliokufa Karibu Na Watu Wema

Wapenzi ndugu waislamu! Ingawaje bila shaka ni ruhusa kuwazika waliokufa pamoja na wanafamilia wao, lakini mtu akibahatika kuzikwa karibu na Walii wa Mwenyezi Mungu, basi ni vyema zaidi.

Imam wa Ahli Sunna, Imam Ahmad Raza Khan رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ amesema, ‘Wazikeni watu wenu waliokufa karibu na watu wema kwasababu kutokana na baraka zao, watu wenu waliokufa hawataadhibiwa ﴿هُمُ الْقَوْمُ لَا يَشْفِي بِهِمْ جَلِيْسُهُمْ﴾ Hawa ni watu ambao hanyimwi mwenye kukaa nao. Pia imetajwa

katika riwaya, ﴿أَذِفُوا مَوْتَكُمْ وَسَطَ قَوْمِ الصَّالِحِينَ﴾ *Wazikeni watu wenu miongoni mwa walio wema.*

(Al-Firdaus bimaSaur-ul-Khattab, juz 1, uk. 102, Hadith 337)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

4. Watu Wa Makaburini Walimjia Katika Ndoto.

Mtu mmoja alikua na mazoea ya kukaa makaburini, ikiletwa jeneza humswalia, na jioni anapotoka husimama kwenye lango la makaburi akiomba kama ifuatavyo: ‘Enyi watu wa makaburini! Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ awape faraja, awe na huruma kwa hali yenu, awasamehe dhambi zenu na akubali matendo yenu mema!’

Yule mtu alisimulia, ‘Jioni moja nilirudi nyumbani na nilisahau kuwaombea. Usiku ule niliona watu wengi katika ndoto yangu. Nikawauliza, ‘Nyinyi ni nani na kwanini mmekuja?’ wakasema, ‘Sisi ni watu wa makaburini. Ulifanya kua mazoea yako kutupatia zawadi kabla ya kurudi nyumbani kila siku na leo hujatupatia.’ Nikauliza, ‘Zawadi hiyo ilikua nini?’ Wakasema ‘Ilikua zawadi ya maombi.’ Kisha nikasema, ‘Sawa, nitawatumia tena zawadi ile.’ Na baada ya hapo sikuacha mazoea yangu (Kuwaombea).’ *(Sharh-us-Sudoor, uk. 226)*

Roho Huja Majumbani Na Huomba Wafikishiwe Thawabu

Wapenzi ndugu waislamu! Kutokana na hili tunajifunza kua waliokufa huwatambua wale wanaokuja makaburini mwao. Na wanapata faida kutokana na dua ya walio hai. Na walio hai wakiacha kuwatumia zawadi ya thawabu basi wanatambua hili na Mwenyezi Mungu **عَزَّوَجَلَّ** huwapa ruhusa kuenda katika nyumba na kuomba wafikishiwe thawabu.

Katika ukurasa wa 650 wa juzu ya 9 ya Fatawa Razawiyyah, A'l Hadrat Imam wa ahli Sunna, mfufuaji wa dini, Imam Ahmad Raza Khan **رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ** amesema: 'Imetajwa katika vitabu 'Gharaib' na 'Khazanah' kua roho za waumini hutembelea majumba kila Alhamisi usiku, siku za Eid , siku za Aashura na usiku wa Nisfu Shaaban na husimama nje ya nyumba zao na kila Roho inaita kwa sauti ya juu na ya huzuni, 'Enyi watu wa nyumba yangu! Enyi watoto wangu! Enyi jamaa zangu! Tafadhalini mtusaidie na mtoe sadaka kwa nia ya kutufikishia sisi thawabu zake.' (*Fatawa Razawiyyah, vol. 9, pp. 650*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

5. Baraka Za Papo Hapo Za Kufikisha Thawabu

Kwa upande wa baraka za papo hapo za kufikisha thawabu, Allama 'Ali Qaari **رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ** amenukuu: Sheikh Akbar

Muhyuddin bin Arabi رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ wakati mmoja alikaribishwa mahali kwa chakula. Alimuona kijana mdogo akila, ambaye alijulikana kua na uwezo wa kujua yanayoendelea ndani ya kaburi. Alipokua akila, ghafla alianza kulia kwa uchungu. Alipoulizwa sababu yake alisema ni kwasababu mama yake alikua anachomeka katika moto wa jahannam. Shaykh Akbar Muhyuddin Bin ‘Arabi رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alikua amesoma Kalimah Tayyibah mara 70,000. Shaykh alimuomba Mwenyezi Mungu moyoni amfikishie thawabu mama yake yule kijana. Mara ghafla kijana alianza kutabasamu na akasema amemuona mama yake peponi. *(Mirqat-ul-Mafatih, Juz. 3, Uk. 222, Hadithi 1142)*

Wapenzi ndugu waislamu! Mmeona? Yule kijana alipewa uwezo wa kuona hali isiyoonekana! Hali ya aliyekufa ilibadilika kabisa kutokana kutumiwa thawabu na Seyidna Bin Arabi. Hadithi inayotaja ubora wa kusoma Kalima Tayyibah mara 70,000 ni kama ifuatavyo: ‘Bila shaka yeyote anayesoma ﴿لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ﴾ mara 70,000 atasamehewa na Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ na yule aliyesomewa pia atasamehewa.’

(Mirqat-ul-Mafatih, Juz. 3, Uk. 222, Hadith 1142)

Sisi pia tunatakiwa tujaribu kusoma Kalimah Tayyibah mara 70,000 angalau mara moja katika maisha. Wale watu ambao wapenzi wao wamefariki watakiwa pia kusoma Kalimah hii na kuwatumia thawabu. Sio lazima kumaliza somo la Kalimah mkao mmoja bali yaweza pia kukamilishwa kidogo kidogo.

Ukisoma mara 100 kila siku basi idadi ya 70,000 itakamilika ndani ya miaka miwili.

Tafsiri Ya Kumuona Mtu Aliyekufa Akiwa Mgonjwa Katika Ndoto

Imesimuliwa kua kuota ndoto ya mtu aliyekufa akiwa katika hali ya hasira, ugonjwa au uchi (nk.) basi mara nyingi hua ni alama ya mtu kuadhibiwa. Kwa hivyo, ikiwa mtu atamuona muislamu aliyefariki katika hali hii, amtumiye Thawabu za amali njema.

Imetajwa katika ukurasa wa 139 ya kitabu chenye kurasa 561 kiitwacho ‘*Malfuzaat-e-A’laHadrat*’ kilichochapishwa na idara ya uchapishaji ya Dawat-e-Islami, Maktaba-tul-Madinah:

Swali: Mtu mmoja alimuona binti yake aliyefariki katika ndoto katika hali ya kua ni mgonjwa na uchi na ameiona ndoto hii mara nyingi.

Jibu: Ikiwa Kalima Tayibah itasomwa mara 70,000 pamoja na swala ya Mtume mwanzo na mwisho na thawabu itumiwe kwa aliyekufa *إِنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ* itakua njia yakuokoka kwa anayesoma na yule anayesomewa, na msomaji atapata thawabu maradufu. Kama atatuma thawabu kwa watu wawili, atapata thawabu mara tatu. Kwa namna hii, thawabu yaweza kutumwa kwa

mamilioni ya waislamu, hata kwa waislamu wote wanaume na wanawake, basi atapata thawabu kiwango cha watu aliyowatumia.

6. Alinikaribia na moto, na kama sio.....

Mtu moja alimuona ndugu yake aliyefariki katika ndoto na akamuuliza, ‘Kulitokea nini baada ya wewe kuzikwa?’ Akajibu, ‘Mtu mmoja alinikaribia na moto, na kama sio dua za walioniombea basi angenichoma bila shaka.’ (*Sharh-us-Sudoor, uk. 281*)

Kwa Maombi Ya Walio Hai, Waliokufa Husamehewa,

Wapenzi ndugu waislamu! Kutokana na hili tunajifunza kua waislamu waliofariki wanafaidika sana kwa maombi ya walio hai. Imetajwa katika ukurasa wa 382 wa kitabu chenye kurasa 448 kilichochapishwa na idara ya uchapishaji ya Dawat-e-Islami, Maktaba tul Madina kiitwacho ‘*Madani Treasure of Blessings*’: Mtume mtukufu wa daraja صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alisema, ‘Uma wangu wataingia makaburini mwao na dhambi zao lakini watatoka makaburini mwao bila dhambi, kwa kua dhambi zao zitasamehewa na maombi ya waumini’

(*Al-Mu’jam-ul-Awsat, juz. 1, uk.509, Hadithi. 1879*)

صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ

7. Baba yake alimjia katika ndoto na akasema

Sayidina Imamu Sufyan bin‘ Uyeina رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ amesema, “Wakati baba alipofariki, nililia kwa uchungu. Nilitembelea

kaburi lake kila siku. Kisha muda ulipopita nilianza kumtembelea kwa uchache. Siku moja baba akaja kwenye ndoto yangu na akasema, ‘Ewe mwanangu! Kwanini unachelewa kuja?’ Nikauliza, ‘Kwani unajua ninapokuja? Akajibu, ‘Kwanini? Ninajua kila unaponitembelea na ninafurahi nikikuona wewe, na vile vile jirani zangu wanafurahishwa na maombi yako.’ Hivyo basi, baada ya ndoto hii, nilianza kuzuru kaburi la marehemu baba kila siku bila kukosa.’ (*Sharh-us-Sudoor, uk. 227*)

9. Aliyoko Ndani Ya Kaburi Ni Kama Anayezama.

Wapenzi ndugu waislamu! Tumejifunza kua waliokufa wanafurahishwa na kutembelewa na rafiki na jamaa zao, kwa maombi yao na kufikishiwa thawabu kutoka kwao na huwangojea wale jamaa ambao hawatembelei. Kipenzi Mtume aliyebarikiwa صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alisema, ‘Hali ya aliyekufa ni kama mtu anayezama, kwakua anangojea kwa hamu Dua ya baba yake, mama, ndugu ama marafiki. Na Dua ya yeyote inapomfikia, basi kwake yeye, ni bora kuliko ulimwengu na kila kitu kilichomo ndani yake. Mwenyezi Mungu mwenye nguvu humpa aliekufa zawadi aliyotunukiwa na jamaa zake katika sura ya milima. Zawadi ya walio hai ni kuwaombea msamaha waliokufa’ (*Shu’ab-ul-Iman, juz. 6, uk. 203, Hadith 7905*)

صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ

Ikiwa makaburi ya wazazi yako katikati ya makaburi, basi....

Wapenzi ndugu waislamu! Bila shaka, waliobahatika kweli ni wale wanaotembelea makaburi ya wazazi wao. Hata hivyo, kumbuka kua kama haiwezekani kufikia makaburi ya wazazi (ama wengine) bila kukanyaga makaburi mengine, basi Fatiha isomwe kwa mbali. Kwasababu kutembelea makaburi ya Mawalii au makaburi ya wazazi ni kitendo cha mustahab (kilichopendekezwa) na kukanyaga kaburi la muislamu ni haramu. Hakuna ruhusa katika Sheria kutekeleza kitendo cha mustahab kupitia kitendo cha haramu. Imam wa Ahli Sunna, Imam Ahmad Raza Khan رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ ameandika katika ukurasa wa 524 wa juzu ya 9 ya *Fatawa Razawiyyah*: Ni muhimu kuzingatia wakati unapotembelea kaburi maalum kua kama hakuna njia isipokua kwa kupitia juu ya makaburi ya waislamu basi hairuhusiwi. Simama kwenye njia kuu kwa mbali kwa kukelekea kaburi lile na uombe.

(Fatawa Razawiyyah, juz 9, uk. 524)

Kuhusu kukaa kando ya kaburi na kusoma Quran Tukufu

Aliulizwa swali Imam Ahmad Raza Khan رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ.

Swali: Je inaruhusiwa kusoma Quran kwenye kaburi?

Jibu: Kusoma Quran moyoni au kwa kuangalia kwenye kaburi inaruhusiwa (kutokana na kusoma Quran baraka zinashuka pale, na roho ya aliyekufa hupata faraja) ikifanywa kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ. Usikae juu ya kaburi, au

kukanyaga juu ya kaburi lolote ili kufikia lile kaburi. Ikiwa kufikia kaburi haiwezekani bila kukanyaga juu ya makaburi mengine, basi ni haramu kuenda karibu kusoma. Bali usome Quran kutoka mbali bila kukanyaga kaburi lolote.

(Fatawa Razawiyah, Juz. 9, Uk. 524-525)

10. Vazi la Nuru

Mcha mungu mmoja alimuona ndugu yake aliyekufa katika ndoto na akamuuliza, 'Je, maombi ya walio hai hukufikia wewe?' Akajibu, 'Ndiyo, naapa kwa Mwenyezi Mungu **عَزَّوَجَلَّ**! Huja katika sura ya vazi la Nuru ambalo kisha tunalivaa'

(Sharh-us-Sudoor, Uk. 305)

صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ

11. Sinia la Nuru

Wapenzi ndugu waislamu! Tumejifunza kua maombi na thawabu zinazotumwa, huwafikia waislamu waliofariki kwa sura nzuri sana kwa rehema ya Mwenyezi Mungu **عَزَّوَجَلَّ**. Kwa hivyo, tunatakiwa tuendelee kutuma thawabu kwa jamaa zetu waliofariki bali kwa waislamu wote.

Imetajwa katika *Sharh-us-Sudoor*: Wakati mtu anapotuma Thawabu kwa waliofariki, Sayidna Jibril **عَلَيْهِ السَّلَام** huiweka kwenye sinia la nuru na huipeleka kwenye kaburi la aliyetumiwa. Na humwambia, Ewe ulioko kaburini! Hii ni

zawadi Jamaa zako wamekutumia, ipokee.’ Anaposikia hili aliyekufa anafurahi sana na majirani wake wanahuzunika kwa kukosa (Neema kama ile)’ *(Sharh-us-Sudoor, Uk. 308)*

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

4. MAUA YA MADANI YA KUTUMA THAWABU

Kaburi Likanawirika

- ❖ Anapotaka mtu kutembelea kaburi la mcha Mungu au kaburi la muislamu yeyote, basi ni Mustahab kuswali rakaa mbili ya swala Nafl (ili mradi isiwe wakati wa makruhu) nyumbani mwake. Katika kila Rakaa asome Ayatul Kursi mara moja na Suratul Ikhlas mara tatu baada ya suratul Fatiha na atume Thawabu ya swala hii kwa mwenye kaburi ambaye amekusudia kumtembelea. Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ ataleta mwangaza katika kaburi la aliyefariki na atampa Thawabu kubwa zaidi Yule aliyetuma Thawabu. *(Fatawa ‘Aalamgiri, juz. 5, uk. 350)*

Kitendo cha kuwafanya waliozikwa wote kua waombezi

- ❖ Mtume Mwenye Rahma صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alisema: yeyote atakayeingia makaburini na asome Suratul Fatiha, Suratul

Ikhlas na Surat Takasur kisha aombe dua ifuatayo, ‘Ewe Mwenyezi Mungu **عَدَّوَجَلَّ**! Yote niliyosoma kutoka kwenye Quran Tukufu, uiruzuku Thawabu yake yote kwa wanaume wote na wanawake wote waislamu waliozikwa katika makaburi haya.’ Basi wote watakua waombezi wake siku ya Kiama.’ *(Sharh-us-Sudoor, uk. 311)*

صَلُّوا عَلَيَّ الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيَّ مُحَمَّدٍ

Njia Ya Kupata Thawabu Idadi Ya Waliofariki

- ❖ Imeelezewa katika hadithi: Yeyoye atakayesoma Suratul Ikhlas mara 11 na atume thawabu kwa waliofariki, atazawadiwa kulingana na idadi ya waliofariki.’

(Jam’-ul-Jawami’ lis-Suyuti, juz 7, uk. 285, Hadithi 23152)

Kutuma Thawabu yaweza pia kua katika njia ifuatayo: Nenda makaburini, soma Suratul Fatiha , kisha kutoka ﴿**الْم**﴾ mpaka ﴿**مُفْلِحُونَ**﴾, Ayatul Kursi, ﴿**أَمَّنَّا لِرَسُولٍ**﴾ mpaka mwisho wa Surah, Surat Yasin , Suratul Mulk, Surat Takasur mara moja na Suratul Ikhlas (Sura kamili) mara 12, 11, 7 au mara 3. *(Bahar-e-Shari’at, juz 1, uk.849)*

صَلُّوا عَلَيَّ الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيَّ مُحَمَّدٍ

12-13. Ghaus-e-A'zam Sayiduna Sheykh 'Abdul Kadir Jaylani رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alipozuru kaburi lilobarikiwa la Imam wake

Ghaus-e-Azam wetu رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alikua Hambali, Kumaanisha alikua Muqalid (mfuasi wa dhehebu la) Imam Ahmad Bin Hambal رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ Ghaus-e-Azam رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alikua na kawaida ya kuzuru makaburi na hasa makaburi yaliyobarikiwa ya Mawalii watakatifu. Sayiduna Sheikh 'Ali Bin Hayti رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ amesema: 'Wakati mmoja nilizuru kaburi liloangazwa la Imamu Ahmad Bin Hambal رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ nikiandamana na Sayiduna Sheikh 'Abdul Kadir Jaylani na Shaykh Baka Bin Batwu رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ, ambapo niliona kua Sayiduna Imam Ahmad Bin Hambal رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ alitoka kutoka kwenye kaburi lake, na akamkumbatia Sheikh 'Abdul Kadir Jaylani رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ, na akampatia vazi la heshima na akasema 'Ewe Abdul Kadir! Watu wote watakutegemea wewe katika ujuzi wa Shari'ah na Tareeqah.'

Kisha nilienda pamoja na Sheikh 'Abdul Kadir Jeilani رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ kwenye kaburi lilobarikiwa la Sayiduna Sheikh Maarufu Karkhi رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ ambapo Sheikh 'Abdul Kadir Jeilani رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alisema, ﴿السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا شَيْخَ مَعْرُوفٍ! عَبْرَتَاكَ بِدَرَجَتَيْنِ﴾ yaani, 'Ewe Sheikh Maarufu! Amani iwe juu yako. Tumetangulia mbele yako kwa ngazi mbili.' Sayyiduna Shaykh Maarufu Karkhi رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ kisha akajibu kutoka kwenye kaburi lake, ﴿وَعَلَيْكَ السَّلَامُ يَا سَيِّدَ أَهْلِ زَمَانِهِ﴾

‘Na amani iwe juu yako, Ewe kiongozi wa watu wa wakati wako.’ (*Qalaaid-ul-Jawahir, Uk. 39*)

Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ awarahamu na atusamehe kwa baraka yao!

أَمِينٍ بِجَاهِ النَّبِيِّ الْأَمِينِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Wapenzi ndugu waislamu! Kutokana na hili twajifunza kua, hata baada ya kuaga ulimwenguni, Walii watakatifu bado wako hai katika makaburi yao yaliyobarikiwa, kama Imamu Ahmad Bin Hambal رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ alivyotoka kutoka kwenye kaburi lake na kumkumbatia Sheikh ‘Abdul Kadir Jeilani رَحِمَهُ اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ. Na Sayiduna Shaykh Maarufu Karkhi رَحِمَهُ اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ akajibu salamu zake kutoka kwenye kaburi lake kwa namna ambayo ilisikika nje.

10 MAUA YA MADANI KUHUSU JINSI YA KUZURU

MAKABURI YA MAWALII

- ❖ Wakati wowote unapozuru kaburi takatifu la Walii, likaribie kutoka miguuni na usogee na usimame mbele ya uso wake kwa umbali wa angalao futi nne na umsalamie kwa sauti ya wastani kama hivi: ﴿السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا سَيِّدِي وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ﴾, alafu soma Swala ya Mtume (Durood Ghausiya) mara tatu, Suratul Fatihah mara moja, Aya tul Kursi mara

moja, Suratul Ikhlas mara saba, Swala ya Mtume (Durood-e-Ghausiya) mara saba, na ikiwa muda utaruhusu, soma suratul Yasin na Suratul Mulk pia. Kisha umuombe Mwenyezi Mungu **عَزَّوَجَلَّ** kwa njia ifuatayo: ‘Ewe Mola niruzuku Thawabu ya kisomo kulingana na ukarimu wako, sio kulingana na matendo yangu, na uitume kama zawadi kutoka kwangu hadi kwa huyu mja wako aliyekubaliwa.’

Kisha uombe unachokitamani kilichoruhusiwa ukipate, Kwa wasila na baraka ya yule mtakatifu aliyekubaliwa na Mwenyezi Mungu **عَزَّوَجَلَّ**. Alafu umsalamie tena kama ilivyo juu kisha urudi. (*Fatawa Razawiyyah, Juzu. 9, Ukurasa wa. 522*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Durood-e-Ghausiyah

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى سَيِّدِنَا وَمَوْلَانَا
مُحَمَّدٍ مَعْدِنِ الْجُودِ وَالْكَرَمِ وَالْإِلَهِ وَبَارِكْ وَسَلِّمْ

(*Madani Treasure of Blessings, uk. 257*)

Kuzuru Makaburi ya Watu Wema ni Sunnah

- ❖ Kipenzi Bwana Mtume aliyebarikiwa صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alikua akizuru makaburi yaliyobarikiwa ya mashahidi wa vita vya Uhud na huwaombea. (*Musannaf 'Abdur Razzaq, juz. 3, uk. 381, Hadithi 6745; Tafseer Durr-e-Mansur, juz 4, uk 640*)

Hupatikana Faida Kwa Kuzuru Makaburi Ya Mawalii.

- ❖ Wanazuoni wamesema, 'Inaruhusiwa kuzuru makaburi yaliobarikiwa ya Mawalii, na hufaidika anayewazuru.'
- (Durr-e-Mukhtar, Juz. 3, Uk.178)*

Usilibusu kaburi

- ❖ Wakati unaenda kuzuru makaburi ya watu wema, usijishughulisha na mazungumzo yasiyo na maana. Aidha usilibusu kaburi au kuwekelea mikono yako juu yake, bali usimame umbali kiasi na kaburi. (*Fatawa Razawiyyah, Juz. 9, Uk. 522-526*)

Njia Ya Kutoa Salamu Katika Makaburi ya Mashahidi

- ❖ Wakati unapozuru makaburi ya mashahidi , toa salamu ifuatavyo:

سَلَامٌ عَلَيْكُمْ بِمَا صَبَرْتُمْ فَنِعْمَ عُقْبَى الدَّارِ

Amani iwe juu yenu kwasababu ya mlivyo subiri, basi ni mema mno malipo ya Nyumba ya akhera!

(Fatawa 'Aalamgiri, Juz. 5, uk. 350)

Kuweka Tandiko Lenye Mapambo Juu Ya Kaburi

- ❖ Inaruhusiwa kufunika makaburi yaliyobarikiwa ya Mawalii kwa nguo yenye mapambo, ikiwa lengo lake ni kujenga heshima ya watu wema katika nyoyo za watu ili waweze kuwaheshimu na wapate baraka kutoka kwao. (*Durr-e-Mukhtar, Juz. 9, Uk. 599*)

Kujenga Kuba juu ya Kaburi

- ❖ Ni bora kutojenga kaburi kwa saruji. Hairuhusiwi kwa sheria ya kiislamu kujenga jengo juu ya kaburi la muislamu wa kawaida kwa kuwa hili ni uharibifu wa mali. Hata hivyo, inaruhusiwa kujenga kuba juu ya makaburi ya Mawalii waliobarikiwa kwa nia njema.

Imesemwa kwenye ukurasa wa 418 ya juzu ya 9 ya *Fatawa Razawiyyah*: Imetajwa katika kitabu cha *Kashf-ul-Ghita*, imeandikwa katika kitabu cha *Matalib-ul-Mu'mineen* kua Salaf (watu wema waliotangulia رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى) walikua wakiona kua inaruhusiwa kujenga jengo juu ya makaburi ya wanazuoni maarufu na mashekhe ili watu waweze kuwazuru na wapate kupumzika ndani yake. Hata hivyo, ikiwa yamejengwa kwa madhumuni ya mapambo na uzuri basi ni Haramu.'

Katika zama za mwanzo, kuba zilijengwa juu ya makaburi ya masahaba رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُمْ katika mji mtukufu wa Madina-

tul-Munawwarah. Ni dhahiri kua ujenzi huu ulitokea tu kutokana na kua watu waliona jambo hili linafaa. Vile vile kuna kuba lililojengwa juu ya mahali patakatifu ambapo Bwana wetu Mtume aliyeheshimiwa صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amepumzika.

Kuwasha Mataa Makaburini

- ❖ Ikiwa kuna faida katika kuwasha mataa kama vile kuna msikiti karibu, au makaburi yako katika njia, au kuna mtu amekaa hapa, au ikiwa kaburi ni la Walii, au mwanachuoni mwenye elimu kubwa, basi mataa yaweza kuwashwa hapa kwa heshima ya roho zao zilizobarikiwa ambazo hungara kama linavyongaa jua, na watu wajue kua hili ni kaburi la muumini mtakatifu, ili wapate baraka kutoka kwalo na wamuombe Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ pale ili maombi yao yakubaliwe. Kitendo hiki kinaruhusiwa na hakijakatazwa. Na vitendo vinategemea nia. (*Fatawa Razawiyyah, Juz. 9, uk. 490; Al-Hadiqa-tun-Nadiyyah, juz. 2, uk. 630*)

Tawaf ya Kaburi

- ❖ Kitendo cha kuzunguka kaburi na nia ya kutoa heshima hakiruhusiwi. (*Bahar-e-Shari'at, juz. 1, Uk. 850*)

Kusujudia Kaburi

- ❖ Kusujudia kaburi kwa kuiheshimu ni haram, na ikiwa utafanya kwa nia ya kuabudu ni Kufuru.

(Fatawa Razawiyyah, Juz. 22, Uk. 423)

14. Kijana Aliyesoma Qurani Tukufu Ndani Kaburi

Abun Nadr Nayshapuri رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ, aliyekua mchimba kaburi mcha Mungu, ameelezea, ‘Siku moja nilichimba kaburi lakini kaburi lililo karibu likafunguka. Nilimuona kijana mmoja aliyevaa mavazi mazuri na ananukia manukato yenye harufu nzuri kabisa amekaa akiwa amekunja miguu huku akisoma Qurani Tukufu. Aliponiona, kijana huyu alisema, ‘Kwani siku ya kiyama ishafika?’ Nikamjibu ‘La.’ Akasema, ‘Uregeshe udongo ulioutoa mahali pake.’ Kwa hiyo nikauregesha mahali pake.’ *(Sharh-us-Sudoor, Uk. 192)*

Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ amrahamu na atusamehe bila hesabu kwa baraka yake!

Wapenzi ndugu waislamu! Mwenyezi Mungu Mwenye nguvu عَزَّوَجَلَّ huhifadhi miili ya Mitume wake عَلَيْهِمُ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ na wacha Mungu watakatifu رَحْمَتُهُمُ اللَّهُ تَعَالَى ndani ya makaburi yao na huwapa neema na fadhila zisizohesabika. Watu kama hawa hata ndani ya makaburi yao huendelea kupata utamu wa ibada ya Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ. Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ husababisha makaburi yao yaliyobarikiwa kua na harufu nzuri na

wakati mwengine hudhihirisha jambo hili kwa watu wengine ili kuwahimiza.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

15. Kaburi Lenye Kunukia

Sayiduna Imam Bin Abi Dunya رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ amepokea kutoka kwa Sayiduna Mughirah bin Habib رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ kua kaburi moja lilikua linanukia. Mtu mmoja alimuota mwenye kaburi lile na akamuuliza, ‘Ni harufu ya nini hii? Jibu lilitolewa, ‘Hii ni harufu ya kusoma Qurani Tukufu na kufunga saumu.’

(Kitabu cha Tahajjud na Kiam-ul-Leil, Juz. 1, Uk.305, Hadithi ya 287)

Wapenzi ndugu waislamu! Kutokana na hili twajifunza kua kuna baraka nyingi katika kusoma Quran Takatifu, Kufunga saumu na vitendo vya ibada, na kua Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ husababisha makaburi ya watiifu wake na waja wake wacha Mungu kua na harufu nzuri kutokana na rehema yake .

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

16. Maiti Chongo

Mcha mungu mmoja رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alisema, ‘Mmoja wa jirani zangu alizoea kutamka kauli potofu. Baada ya kifo chake, nilimuona kwenye ndoto na nikaona hali ya kua ni chongo.

Nikamuuliza, ‘Kulitokea nini?’ Akanijibu, ‘Nilikua nikiwatolea aibu Masahaba wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ basi Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ alinifanya mimi niwe mwenye aibu!’ Baada ya kusema hivyo, alijifunika jicho lake lenye chongo kwa mkono wake’ (*Sharh-us-Sudoor, uk. 280*)

Kila Sahaba Wa Mtume Ni Mtu Wa Peponi.

Wapenzi ndugu waislamu! Kutokana na maelezo haya twajifunza kua ni hatari sana kuwapa makosa Masahaba wa Mtume waliobarikiwa رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُمْ. Acha kando kusema kwa ulimi, mtu hatakiwi hata kufikiria vibaya kuwahuu wao moyoni. Katika ukurasa wa 252 wa kitabu chenye kurasa 1250 kilichochapishwa na idara ya uchapishaji ya Dawat-e-Islamia, Maktaba-tul-Madina, kiitwacho ‘Bahar-e-Shari’at’, Mufti Muhammad Amjad ‘Ali A’zami رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ amesema, ‘Masahaba wote waliobarikiwa رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُمْ ni watu wema na wacha Mungu, na ni waadilifu. Ni lazima watajwe kwa uzuri wakati wanapotajwa.’

Yeye رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ amesema zaidi katika ukurasa wa 254 ‘Masahaba wote waliobarikiwa رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُمْ, wenye daraja ya juu na ya chini (ingawa hakuna mwenye daraja ya chini kati yao) wamejaaliwa pepo. Licha ya kuingia katika moto wa jahannam, hata hawatosikia sauti ya moto wa jahannam na watabakia katika neema na starehe milele. Msiba mkubwa wa siku ya hukumu haitowapa huzuni yoyote na siku hiyo malaika

watawakaribisha, wakisema hii ni siku mliaoahidiwa. Hili limetajwa katika Qurani Tukufu.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

17. Mfungwa Katika Kisima Cha Kiajabu

Shayban Bin Hasan amesema: ‘Baba yangu na ‘Abdul Waahid Bin Zayd, walikwenda kushiriki katika jihadi (vita). Walipokua njiani, waliona kisima cha ajabu ambamo walisikia makelele. Walipochungulia wakamuona mtu mmoja amekaa kwenye kiti na maji yakipita chini yake. Wakamuuliza ‘Wewe ni binadamu au jinni?’ Akajibu, ‘Binadamu’. Wakamuuliza, ‘Watoka wapi?’ Akajibu, ‘Antakiyah.’ Kisha akasema, ‘Kisa changu ni kwamba nilifariki na sasa nimefungwa katika kisima cha ajabu kwasababu ya deni ambalo sikulipa. Ingawaje watu wa Antakiyah wananzungumzia vyema, lakini hakuna aliyelipa madeni yangu.’

Basi, wote wawili walienda Antakiyah na wakawatafuta waliokuwa wakimdai na wakalipa deni lake na wakarudi pale mahali. Walipofika hawakumuona yule mtu wala kisima chenyewe. Walipolala usiku pale mahali kisima kilipokuweko, waliota ndoto ambapo yule mtu alikuja na akasema, ﴿جَزَاكُمَا اللَّهُ عَنِّي خَيْرًا﴾ yaani Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ awajazie nyote wawili kheri kutoka kwangu mimi. Baada ya madeni yangu kulipwa yote, Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ ameniweka peponi. (*Sharh-us-Sudoor, uk. 267*)

Hata Shahidi anayedaiwa madeni hataingia peponi mpaka....

Wapenzi ndugu waislamu! Kutokana na hili tunajifunza kua deni ni kwa hakika mzigo mzito kubeba. Wale wanaochelewa kulipa madeni yao wazingatie kisa hiki na badala ya kuwatesa waliowakopesha, waende kwao kulipa deni na watoe shukrani zao kwao. Usije ukaendelea kuchelewesha mpaka kifo kikakufikia na ukapata shida katika kaburi lako.

Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, ‘Naapa kwa yule ambaye roho yangu iko mikono mwake!’ Ikiwa mtu ameuliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ na kisha akapewa uhai tena, akauliwa tena na ana mzigo wa deni juu ya kichwa chake, hataingia peponi hadi deni lake lilipwe.’

(Musnad Imam Ahmad, juz. 8, uk. 348, Hadithi 22556)

Ikiwa muislamu amefariki katika hali ya kua anadaiwa basi wale walioko karibu naye watakiwa walipe deni lake mara moja, ili maarehemu afanyiwe wepesi katika kaburi lake. Mtume wa Rehema صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, ‘Bila shaka, mwenzenu amesimamishwa katika mlango wa pepo kwasababu ya madeni. Ikiwa mnataka mnaweza kulipa deni lake lote, na ikiwa mnataka mnaweza kumuacha yeye (yaani marehemu mwenye madeni) aadhibiwe.’ *(Al-Mustadrak, Juz. 2, Uk. 322, Hadithi 2260-61)*

صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ

Kutoa Tangazo Kabla Ya Swala Ya Jeneza

Wapenzi ndugu waislamu! Itakua bora ikiwa Imam au ndugu wa kiislamu aweze kutoa tangazo lifuatalo kabla ya Swala ya Jeneza: ‘Jamaa na marafiki wa marehemu, Tafadhalini sikizeni kwa makini ikiwa marehemu aliwahi kukuudhi au kunyima haki zako basi tafadhali msamehe, إِنَّ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ, marehemu atafaidika na wewe pia utapata thawabu. Baada ya hili Imam aeleze nia na namna ya kuswali Swala ya Jeneza.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

18. Alifungua macho ndani ya kaburi.

Sayiduna Abu ‘Ali Sayyiduna Abu ‘Ali رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ amesema: ‘Niliuweka mwili wa mcha Mungu ndani ya kaburi, na nilipomfungua sanda na nikakiweka kichwa chake juu ya ardhi ili Mungu عَزَّوَجَلَّ amuonee huruma kwa hali yake, yule mcha Mungu alifungua macho yake na akaniambia, ‘Ewe Abu Ali unanidhalilisha mbele ya Mugu wangu ambaye ni karimu juu yangu! Nikasema, ‘Ewe bwana wangu! Kuna uhai baada ya kifo?’ Akajibu, ﴿بَلْ أَنَا حَيٌّ وَكُلُّ مُحِبِّ اللَّهِ حَيٌّ لَأَنْصُرَنَّكَ بِجَاهِي عَدَا﴾ Bali mimi niko hai na kila mtu ambaye ni kipenzi cha Allah yuko hai. Bila shaka kwa cheo na heshima nitakazopewa siku ya kياما, nitakusaidia.’ (Fatawa Razawiyyah, Juz.9, Uk. 433)

Marafiki Wa Mwenyezi Mungu Wako Hai Hata Baada Ya Kufa

Wapenzi ndugu waislamu! Kutokana na hili twajifunza kua mashahidi waliobarikiwa na marafiki wa Mwenyezi Mungu wako hai katika makaburi yao na wanafahamu kila kitu. A’la Hadrat رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ: amesema ‘Alamah ‘Ali Qaari رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ ameandika katika Sharhe *Mishkat*, ‘Kwa hakika hakuna tofauti baina ya hali hizi mbili (yaani maisha na kifo) kwa marafiki wa Mwenyezi Mungu. Kwa sababu hii, inasemekana kua hawafi, bali huhamishwa kutoka nyumba moja kuenda kwa nyingine.’ (*Fatawa Razawiyyah, juz. 9, Uk. 433; Mirqat-ul-Mafatih, Juz.3, Uk. 459, Hadithi 1366*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

19. Kwato Ya Ng’ombe Ilipokwama Kwenye Ardhi....

Kukata nyasi zilizokauka kutoka makaburini na kuzichukua inaruhusiwa, lakini hairuhusiwi katika sheria kuacha wanyama watembe au walishe juu ya makaburi. A’la Hadrat, Imam wa Ahli Sunna, Imam Ahmad Raza Khan رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alisema, ‘Mimi (Mwenyezi Mungu anisamehe) nilisikia kutoka kwa mwenzangu Sayyidi Abul Husein Nuri مَدَّ ظِلُّهُ الْعَالَى ya kua kuna pahali panapoitwa Ganj –e-Shahidan (ambapo pana mashahidi wengi wamezikwa) katika mwitu karibu na Mareharah Mutahharah (Hindi). Mtu mmoja alipita huku akitembea

juu ya makaburi na ng'ombe wake. Kulikua na baadhi ya eneo laini kwenye ardhi na ghafla kwato ya ng'ombe ilisakama kwenye ardhi na ikagunduliwa kua kulikua na kaburi hapo. Sauti ilitoka kwenye kaburi, 'Ewe Mtu, umeniudhi, kwa kua guu la ngombe wako limenikanyaga kifuani mwangu.' (*Fatawa Razawiyah, Juz. 9, Uk. 453*)

Wapenzi ndugu waislamu! Tumejifunza kuwa mashahidi wako hai na miili yao imebaki mizima kaburini.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

20. Onyo Kwa Yule Aliyekaa Juu ya Kaburi.

'Umarah Bin Hazm رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ amesema: Kipenzi Mtume na aliyebarikiwa صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ aliniona nimekaa juu ya kaburi na akasema, 'Ewe ulioko juu ya kaburi! Shuka kutoka kwenye kaburi. Wewe usimuudhi yeye na yeye asikuudhi wewe,'

(*Fatawa Razawiyah, Juz. 9, Uk. 434*)

Kutokana na maelezo haya ya madani, wanatakiwa wazingatie wale wanaoshindikiza jeneza makaburini na wanakaa juu ya makaburi bila kujali wakati wa kuzikwa maiti.

21. Alipokanyaga Kaburi Alisikia Sauti

Sayiduna Kasim Bin Mukhaymar رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ amesema: Wakati mmoja mtu aliweka mguu wake juu ya kaburi, ambapo alisikia sauti imetoka ndani ikisema, ﴿إِلَيْكَ عَنِّي وَلَا تُؤْذِنِي﴾, ‘Ondoka na usiniudhi mimi!’ (Ibid, Uk. 452; Sharh-us-Sudoor, Uk.301)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

22. Mwenye Kaburi Alizungumza Na Mtu Aliyelala Juu Ya Kaburi

Sayiduna Abu Kilabah رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ amesema: Nilisafiri kutoka Syria mpaka Basra (Iraq), na usiku mmoja nilishuka kwenye mtaro, nikashika Wudhu na nikaswali rakaa mbili za swala ya Nafl. Kisha nikaegemeza kichwa changu juu ya kaburi na nikalala. Nilipoamka, ghafla nilisikia aliyelikwa katika kaburi lile akilalamika na akisema, ﴿لَقَدْ أذَيْتَنِي مِنْذُ اللَّيْلَةِ﴾ yaani, ‘Umeniudhi usiku mzima. Tunajua na nyinyi hamjui, hatuna uwezo wa kutenda mema. Rakaa mbili za swala ya Nafl ulizoswali ni bora kuliko ulimwengu na kilichomo ndani yake.’ Kisha akasema zaidi, ‘Ewe Mola عَزَّوَجَلَّ wajazie kheri wanaoishi duniani. Wanapotuma thawabu kwetu, tunaletewa thawabu zile kwa sura ya milima ya nuru.’ (Fatawa Razawiyyah, uk. 452; Sharh-us-Sudoor, uk. 305)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

23. Inuka! Umeniudhi!

Sayiduna Bin Mina Taabii رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ ameelezea, ‘Wakati mmoja, nilienda makaburini, nikaswali rakaa mbili kisha nikajilaza juu ya kaburi. Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ! Nilikua macho kikamilifu niliposikia yule aliyetikwa akisema, ﴿قُمْ فَقَدْ أَدَيْتَنِي﴾ ‘Inuka! Umeniudhi!’ (*Dalaail-un-Nubuwwah, Juz. 7, Uk. 40*)

Kukanyaga Kaburi Ni Haramu

Wapenzi ndugu waislamu! Kutoka maelezo ya 21, 22, 23, tunajifunza kua kukanyaga au kulala juu ya kaburi huwaudhi waliozikwa. Na kumuudhi muislamu ni Haram na ni kitendo kitakachomtia mtu motoni. Kwahivyo, usiweke mguu kwenye kaburi ya muislamu yeyote, usilikanyage, usilikalie, usilitegemee, kwasababu hili limekatazwa na Kipenzi Mtume aliyebarikiwa صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Hapa kuna misemo miwili ya Mtume wa Rehema صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ:

- ❖ Ni heri kutembea kwenye makaa ya moto, au kwenye makali ya upanga au miguu yangu ishonwe kwenye viatu vyangu kuliko kutembea juu ya kaburi la Muislamu yeyote. (*Sunan Ibn Majah, Juz. 2, Uk. 250, Hadithi 1568*)
- ❖ Ni bora kwa mtu kukaa juu ya makaa ya moto mpaka ichome nguo zake na kufika kwenye ngozi yake kuliko kukaa juu ya kaburi. (*Sahih Muslim, Uk.. 483, Hadithi 971*)

Ni Haramu Kutembea Kwenye Njia Iliyojengwa Kwa Kubomoa Makaburi

Tumia njia ya kawaida ya makaburini na usitembee katika njia iliyotengezwa upya. Imetajwa katika kitabu cha *Rad-dul-Muhtar*: Ni Haramu kutembea kwenye njia iliyotengezwa upya kwa kubomoa makaburi. (*Rad-dul-Muhtar, Juz. 1, Uk. 612*)

Bali hata wakati kuna shaka kuhusu ile njia mpya, hairuhusiwi na ni dhambi kutembea juu yake. (*Durr-e-Mukhtar, Juz. 3, Uk. 183*)

Ni Haram Kutembea Kwenye Sakafu Jirani Ya Makaburi Ambayo Imetengenezwa Kwa Kubomoa Makaburi

Imeonekana katika makaburi mengi ya Mawalii, kingo mpya na sakafu zajengwa kuhudumia wageni kwa kubomoa makaburi ya waislamu. Ni haram kulala juu yake, kutembea, kusimama na hata kusoma Zikri au kusoma Quran kwenye sakafu kama hii. Fatiha isomwe kwa mbali.

Kuweka uchafu karibu na kaburi

Kujenga nyumba juu ya kaburi, kukaa au kulala juu ya kaburi, kukojoa au kukidhi haja kubwa juu yake ni vitendo ambavyo vina karaha kubwa na viko karibu na Haramu. Kipenzi Mtume aliyebarikiwa صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, ‘Maiti huudhika ndani ya kaburi kwa mambo ambayo alikuwa akiudhika nayo nyumbani mwake.’ (*Al-Firdaus bimaSaur-ul-Khattab, Juz. 1, Uk. 120, Hadithi 749*)

Ikiwa Mtu Anahitaji Kukanyaga Kaburi Wakati wa Kumzika Maiti Basi....?

Wakati wa kuenda kuchimba kaburi au kuzika maiti, kama kuna makaburi njiani, basi kwa hali hii ya dharura ruhusa itatolewa kukanyaga juu ya makaburi. Hata hivyo, jaribu sana kujizuia kutokana na hili kadri iwezekanavyo na fanya hivi bila viatu, huku ukiwaombea msamaha waliozikwa katika makaburi hayo. (*Fatawa Razawiyyah, juz 9, Uk. 447*)

Katika hali kama hii, wale watu wanaotakiwa kuzika peke yao ndio waende na hata asiweko mtu mmoja wa ziada. Kwa mfano, ikiwa inajulikana watu watatu watatosheleza basi mtu wanne asiende. Ikiwa watu hao watatu inawabidi kusimama juu ya kaburi kwa dharura, basi wanatakiwa kurudi mara moja baada ya kuzika na wasingojee Fatihah n.k. Na wasome Fatihah na dua sehemu ambapo kuna uhakika kuwa hakuna kaburi chini ya miguu.

Kuwalisha Vyakula Vitamu Chungu Makaburini.

Imetajwa katika kurasa za 329-348 za kitabu chenye kurasa 561 kilicho chapishwa na idara ya uchapishaji ya Dawat-e-Islami, Maktaba tul Madinah, kiitwacho *Malfuzaat-e-A'laHadrat:*

Swali: Ni hukumu ipi iliyoko kwa mtu kuchukua vyakula vitamu au sukari makaburini ili awalishe chungu?

Jibu: Wanazuoni wamekataza kuchukua mkate makaburini, vile vile vyakula vitamu. Ama kuwalisha chungu unga, peremende, au sukari kwa nia kua sababu hii chungu hawataudhuru mwili wa aliyekufa ni ujinga mkubwa. Hata bila nia hii, ni bora kugawanya mkate miongoni mwa wacha mungu maskini badala ya kuwapa chungu. Yeye رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ kisha akaendelea kusema, ‘Toa sadaka kwa wingi unavyotaka nyumbani kwako; Imeonekana mara nyingi wakati wa kugawanywa sadaka makaburini, wanawake na watoto wanapiga kelele na kukanyaga juu ya makaburi ya waislamu.

Kunyunyiza Maji Kwenye Makaburi

Usiku wa Nisfu Shaaban au wakati mwengine wa kuzuru makaburi, watu wengine wana desturi ya kunyunyiza maji kwenye kaburi la wanaempenda bila maana; Hili ni israf (kupoteza maji) na haliruhusiwi. Ikiwa mtu afikiria hili litaleta ubaridi kwenye kaburi la marehemu basi pamoja na israf ya (kupoteza) maji ni ujinga mkubwa. Hakuna ubaya kunyunyiza maji baada ya kuzika, bali ni bora. Sawa pia ikiwa kuna mimea yoyote kwenye kaburi na maji yametiwa kwa ajili ya mimea basi hakuna madhara kwa hili. Hata hivyo, ikumbukwe kua ikiwa makaburi yatakanyagwa ili kutiwa maji basi yeyote afanyae hivi atakua anatenda dhambi, na katika hali kama hii, pia usimlipe mtu mwengine kukufanyia kazi hii.

Kuna Hukumu Gani Kujenga Nyumba Katika Makaburi ya Zamani?

Makaburi ni wakfu na kujenga nyumba ya makazi ya kibinafsi ni matumizi ya mali ya umma yasiyofaa na kuifanya ya matumizi ya kibinafsi ni Haramu. Na ikiwa kuna makaburi katika eneo la ardhi na alama zake zimepotea kabisa, basi itakua ni mkusanyiko wa vitendo vya Haramu, yaani kukanyaga makaburi (yasiyo tambulika), kutembea juu yake, kukaa juu yake, kuyakojolea na kutia choo kikubwa; yote hayo ni Haramu. Katika hili kuna aina tofauti za maudhi kwa hawa waislamu na ni waislamu gani hawa? Waliokufa, ambao hawawezi kulalamika na hawawezi kulipa kisasi duniani.

Kumuudhi muislamu ni kama kumuudhi Mwenyezi **عَزَّوَجَلَّ** na Mtume wake **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ**, na mwenye kumuudhi Allah **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** anastahiki kuingia moto wa jahannam. Vile vile ikiwa mtu amejenga nyumba karibu na makaburi, na ameelekeza mtaro wa maji machafu moja kwa moja hadi makaburini, pia ametenda tendo la haram. Na yeyote mwenye uwezo wa kumkataza na asimkataze pia atakua anafanya Haramu. Zaidi, anayeruhusu hili kutokana na tamaa ya kukusanya pesa za kodi ni kama ambaye anapanga mpango wa kununua sehemu katika moto wa jahannam. Mambo haya yaweza kufanyika na mtu ambaye hathamini uislamu, haheshimu waislamu, hamuogopi Mungu **عَزَّوَجَلَّ**, na hajali kifo. ﴿وَالْعِيَادُ بِاللَّهِ تَعَالَى﴾

(Fatawa Razawiyyah, luzu ya 9, ukurasa wa 409)

Ikiwa Mifupa Imeonekana Katika Kaburi La Zamani...?

Ikiwa kaburi limefunguka kutokana na mvua ama sababu nyengine yoyote na mifupa ya maiti yanaonekana, basi ni lazima kulifunika kaburi lile. Suala hili limetajwa katika *Fatawa Razawiyyah*:

Swali: Ni uamuzi upi ambao wasomi wa kiislam wametaja kuhusu hali ambayo kaburi linafunguka, na mifupa ya maiti inaonekana? Katika hali hii, inaruhusiwa au hairuhusiwi kufunika kaburi kwa udongo?

Jibu: Katika hali hii, Sio ruhusa pekee kufunika kaburi kwa udongo bali ni Wajibu (lazima), kwani ni lazima kumstiri Muislamu. (*Fatawa Razawiyyah, Juz.9, Uk. 403*)

Hukumu ya Kufungua Kaburi Katika Misingi ya Ndoto

Wakati mwingine waliokufa huja kwenye ndoto na kusema, 'Niko hai! Nitoe nje! au aseme, maji yamejaza kaburi langu, niko na shida hapa, uhamishe mwili wangu mahali pengine n.k. Hata ikiwa ndoto kama hizi zimeonekana na kurudia tena, hairuhusiwi kufukua kaburi kwa msingi wa ndoto. Kwa hali yoyote, ikiwa mtu alifukua kaburi kwa misingi ya ndoto na mwili wa aliyekufa ukatoka salama pamoja na sanda yake, na harufu nzuri zikanukia, na ishara nzuri nyingine zikonekana, bado yule aliyefukua kaburi bila ya ruhusa ya sharia

atahesabiwa kuwa ni mwenye dhambi. Katika suala hili, soma swali lilfuatalo na jibu lake kutoka *Fatawa Razawiyyah*:

Swali: Kulikuwa na mwanamke ambaye, baada ya kukamilika kwa mda wa uja uzito, alikufa katika mazazi. Alizikwa kulingana na desturi za kawaida, lakini mtu mcha mungu aliona katika ndoto kua amemzaa mtoto aliye hai ndani ya kaburi. Je kwa kuamini ndoto ya yule mtu, inaruhusiwa kufukua kaburi ili kumtoa mtoto pamoja na mwanamke?

Jibu: Hairuhusiwi; isipokua kukiwa na ushahidi wazi. Ndoto ni za aina mbalimbali; imetajwa katika Sirajiyah pia katika *Hindiyah*: mwanamke mmoja ilikua imempita miezi saba ya uja uzito na mtoto alikua anageuka kwenye tumbo. Mwanamke alikufa (kabla ya kuzaa) na akazikwa. Kisha mtu mmoja akamuona kwenye ndoto yule mwanamke akisema, ‘Nimemzaa mtoto’; katika hali hii kaburi halitochimbuliwa, ﴿وَاللَّهُ تَعَالَىٰ أَعْلَمُ﴾ n.k. Mweneyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ ni mweney kujua zaidi.

(*Fatawa Razawiyyah, Juz. 9, Uk. 405-406*)

Soma swali na jibu lifuatalo muhimu sana kuhusu kufukua makaburi kutoka kurasa 501–503 za kitabu cha *Malfuzaat-e-A’laHadrat*:

Swali: Kaburi halina saruji na maji yanajaza kaburi kunaponyesha. Inaruhusiwa kuziba kabisa panapoingia maji.

Jibu: Hakuna madhara katika kuziba kaburi. Lakini hata hivyo halisurhusiwi kuchimbuliwa. Anapozikwa maiti na udongo umewekwa juu yake, anakuwa ni amana ya Mwenyezi Mungu **عَزَّوَجَلَّ** na hairuhusiwi kulifukua. Hii ni kwasababu aliyefariki yuko katika hali moja kati ya mbili ndani ya kaburi; aidha anateseka kwa adhabu, au anafurahia neema. Kama anateseka kwa adhabu, basi yule atakayemuona atakuwa na dhiki kwa hili na hawezi kumfanyia lolote, na kama aliyefariki anafurahia neema, basi aliyefariki atahisi dhiki (likifukuliwa kaburi lake).

Watoto Kucheza Juu ya Kaburi

Mwenye kukusanya kitabu cha *Malfuzaat-e-A'laHadrat*, mtoto wa A'la Hadrat Tajdar-e-Ahl-e-Sunnat, Mufti-e-A'zam Hind 'Allamah Mustafa Raza Khan **رحمتهُ اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ** ameandika katika ukingo kuelezea jibu la A'la Hadrat **رحمتهُ اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ**: Ikiwa ni hali ya kwanza (yaani mateso ya adhabu, Mwenyezi Mungu atuepushie) basi dhiki itakua kubwa zaidi, na kumuudhi muilslamu bila sababu ni haramu, haswa kumsumbua aliyefariki. Zaidi, imethibitishwa katika hadithi 'Aliyefariki husumbuliwa hata na mtu aliyetegemea kaburi.' Kwa hivyo, **مَعَادُ اللهِ عَزَّوَجَلَّ** ukitumia jembe kulichimba bila umuhimu wowote, tu kupenda mwenyewe bila ya dharura, basi maudhiko ya marehemu yatakuaje!

Lo! Hali mbovu ilioje ya makaburi ya waislamu siku hizi! Watu wanakaa juu ya makaburi na kuvuta sigara, wanafanya vitendo viovu, wana mazungumzo yakipuuzi, na wakicheka kwa sauti.

Hili halifanywi na watu wa dini nyengine; Waislamu wenyewe wanatenda vitendo hivi vya kuaibisha. Watoto wanacheza wakizunguka makaburini, na hata punda na mbuzi wanatia choo juu yake, ﴿وَلَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ﴾. Enyi waislamu! Fungueni macho yenu kwa ajili ya Allah عَزَّوَجَلَّ! Nyinyi pia mutauacha ulimwengu siku moja. Kama hamuchukui hatua kwa ajili ya aliyefariki, basi angalau chukueni hatua kwa ajili yenu wenyewe.

24. Aliyefukua Kaburi Akawa Kipofu

Kuna matokeo ya kutisha kutokana na kufukua kaburi bila ya mahitaji ya sheria. Kwa suala hili, imeandikwa katika ukurasa wa 502 wa kitabu cha *A'la Hadrat*: Mara moja 'Allamah Taash Kubra Zaadah رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alisoma hadithi ambayo ilisema, 'Udongo wa makaburi hauli miili ya wasomi.' Shetani alimnongonezea ndani ya moyo wake, 'Mwalimu wangu alikua msomi mkubwa sana. Nichimbue kaburi lake niangalie hali aliyoko! Mnongono huo ulimghilibu kiasi ambacho usiku mmoja alienda makaburini na akafukua kaburi. Aliona kua hata sanda haikuchafuka, Baada ya kuona hivyo, sauti ilitoka kaburini, 'Umeshiona!, Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ akufanye kipofu!' wakati huo huo macho yake mawili yakapofuka.

25. Mtu Aliyefukua Kaburi Alizikwa Akiwa Hai

Kuna kisa kingine cha matokeo mabaya ya mtu ambaye alifungua kaburi kinyume cha sheria. A'la Hadrat رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ

amesema: Alikufa mwanmke mmoja na akazikwa. Mume wake alimpenda sana na upendo huu ulimlazimisha kufikiria kufungua kaburi lake kuona hali gani aliyokua nayo. Alielezea nia hiyo kwa msomi mmoja naye akamzuia kufanya hivyo. Hata hivyo, hakufuata tahadhari hiyo na alimlazimisha kuenda naye makaburini. Msomi alijaribu awezavyo kumzuia, lakini aliendelea kulifungua kaburi na yule msomi alibaki amekaa kando ya kaburi.

Yule mtu alishuka ndani ya kaburi na akaona miguu ya yule mwanamke miwili imefungwa katika nywele zake. Alijaribu sana kuifungua lakini hakuweza kufanya hivyo, kwani ni nani anayeweza kufungua fundo lililofungwa na Mwenyezi Mungu **عَزَّوَجَلَّ**. Yule Msomi alimzuia tena lakini hakukubali. Alitumia nguvu zake mara ya pili, msomi alimzuia tena akimuelezea kua ni bora kumuacha vile alivyo. Akasema, ‘Niache nitumie nguvu zangu mara ya mwisho kisha tutaona kitakacho kua.’ Aliendelea kutumia nguvu zake, ghafla ardhi ilifunguka na yule mtu na mwanamke aliyekufa wote wakazama ndani ya ardhi.

﴿وَالْعِيَّادُ بِاللَّهِ تَعَالَى﴾

صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ

Hukumu Ya Kuzika Kwa Muda Mfupi

Baadhi ya watu wakifa wakiwa mbali na mji wao, huzikwa kwa muda mfupi kisha wanatolewa na kuhamishwa hadi katika mji

wao ili wakazikwe pale. Kufanya hivi hairuhusiwi. Katika jibu la swali linalohusu hili A'laHadrat رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ amesema 'Hili ni haramu; hairusiwi kufungua kaburi baada ya kuzika.'

(Fatawa Razawiyyah, Juz. 9, Uk. 406)

Kuzika Bila Ruhusa Katika Kiwanja Cha Mtu.

Ikiwa mtu atamzika maiti katika kiwanja au shamba bila ruhusa ya mwenyewe, basi mwenyewe ana hiari ya kuutoa mwili au kutandaza ardhi na kuendelea kulima au kujenga juu yake. Kwa suala hili wanavyuoni wanasema, 'Marehemu asifukuliwe baada ya kuzikwa isipokua kwa kutimiza haki ya mtu. Kwa mfano, ikiwa ni kwenye ardhi ambayo ilikua imechukuliwa (kwa dhulma) basi mwenyewe atakua na mamlaka ya kuutoa mwili au kutandaza kaburi mpaka chini.'

(Fath-ul-Baari, Juz. 3, Uk. 170)

Katika jibu la swali kuhusu suala hili, A'la Hadrat رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ amesema akimnasihi mwenye kiwanja, 'Hii ndio hukumu ya kisheria (yaani kuna ruhusa katika sheria kufanya hivyo), lakini Muislamu atakiwa awe mnyenyekevu moyoni, na mwenye huruma kwa waislamu wengine, haswa kwa waliofariki. Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ amesema:

Na wanahurumiana wao kwa wao.

رُحَمَاءُ بَيْنَهُمْ

(Juzuu. 26, Surah Al-Fath, aya. 29)

Ikiwa atasamehe (na aruhusu miili iliyozikwa kinyume cha sheria ibakie katika ardhi yake) basi Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ atasamehe dhambi za mwenye ardhi:

أَلَا تُحِبُّونَ أَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَكُمْ^ط

Je nyinyi hampendi mwenyezi Mungu akusameheni?

(Juzuu ya 18, Surah An-Noor, aya 22)

Ikiwa atamfanyia wema marehemu ndugu yake basi Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ atamfanyia yeye wema: ﴿كَمَا تَدِينُ تَدَانُ﴾ yaani utakavyofanya, sawa litafanywa kwako. Ikiwa atajizuia kutotoa siri ya marehemu ndugu muislamu basi Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ pia ataficha makosa yake: ﴿مَنْ سَتَرَ سَتَرَهُ اللَّهُ﴾ Yaani yeyote atakayemsitiri mtu, Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ atamstiri yeye. Ikiwa ataheshimu kaburi la marehemu nduguye basi Allah عَزَّوَجَلَّ atambariki yeye na heshima katika maisha yake na kifo chake: ﴿اللَّهُ فِي عَوْنِ الْعَبْدِ مَا كَانَ الْعَبْدُ فِي عَوْنِ أَخِيهِ﴾ yaani Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ humsaidia mtu ambaye humsaidia ndugu yake. ﴿وَاللَّهُ تَعَالَى أَعْلَمُ﴾ (Fatawa Razawiyyah, Juz. 9, Uk. 379-380)

صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ

Kitu Gani Chatakiwa Kufanywa Ikiwa Mali Imezikwa Pamoja Na Maiti?

Ikiwa mali ya mtu au pesa zilizikwa pamoja na maiti, basi inaruhusiwa kufukua kaburi ili kuzitoa. Kwa suala hili, wasomi wa fikih wamesema, 'Ikiwa mmoja wa warithi alimzika mwanamke pamoja na vitu vya mapambo bila ya ruhusa ya warithi wengine, basi wale warithi wengine waruhusiwa kufukua kaburi. Ikiwa pesa za mtu zilianguka kwenye kaburi na akakumbuka baada ya kuzika basi inaruhusiwa kufukua kaburi na kuzichukua, hata kama thamani yake ni dirhamu moja' (*Fatawa 'Aalamgiri, Juz. 1, Uk. 167*)

MAELEZO 14 KUHUSU KUZURU MAKABURI

- ❖ Kuzuru makaburi ya waislamu ni Sunnah na kuzuru makaburi yaliyobarikiwa ya Mawalii na mashahidi ni wema zaidi. Kuwapelekea thawabu ni kitendo cha thawab.

(*Fatawa Razawiyyah, juz. 9, uk. 532*)

Jinsi ya Kutoa Salamu Makaburini

- ❖ Simama kando ya kaburi kwa namna ya kua mgongo wako unaelekea kibla na uso wako unaelekea nyuso za wenye kaburi. Kisha, toa salamu kama ilivyotajwa katika hadithi katika kitabu cha *Tirmizi*:

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا أَهْلَ الْقُبُورِ
يَغْفِرُ اللَّهُ لَنَا وَلَكُمْ أَنْتُمْ سَلَفُنَا وَنَحْنُ بِالْآثَرِ

Tafsiri: Salamu ziwe nanyi, Enyi watu wa kaburi! Mwenyezi mungu atusamehe sisi na awasamehe nyinyi. Mumetutangulia na sisi tutawafuata. (Sunan-ut-Tirmizi, Juz. 2, Uk. 329, Hadihi 1055)

Dua Ya Kusababisha Kupata Maombi Ya Msamaha Kutoka Kwa Watu Mamilioni Waliofariki

- ❖ Yeyote aingiaye makaburini na kusoma hii dua:

اللَّهُمَّ رَبَّ الْأَجْسَادِ الْبَالِيَةِ وَالْعِظَامِ النَّخِرَةِ الَّتِي خَرَجَتْ
مِنَ الدُّنْيَا وَهِيَ بِكَ مُؤَمَّنَةٌ أَدْخِلْ عَلَيْهَا رَوْحًا مِّنْ عِنْدِكَ
وَ سَلَامًا مِّنِّي

Tafsiri: Ewe Allah (عَزَّوَجَلَّ)! Mola wa miili iliyooza na mifupa iliyobunguliwa ya walioondoka kutoka ulimwengu huu katika hali ya kukuamini wewe, warahamu na uwape salamu zangu.

Waumini waliokufa kutoka wakati wa Sayiduna Adam عَلَيْهِ السَّلَام mpaka wakati wa maombi hayo wote watamuomba msamaha aliyesoma dua. (*Sharh-us-Sudoor, Uk. 226*)

- ❖ Ikiwa wataka kukaa kando ya kaburi tia maanani hadhi ya aliyezikwa na ukae kwa heshima. (*Durr-e-Mukhtar, juzu 3, Uk. 179*)

Muda unaopendelewa kuzuru makaburi

- ❖ Siku nne bora za kuzuru makaburi ni: Jumatatu, Alhamisi, Ijumaa na Jumamosi. (*Fatawa 'Aalamgiri, juz 5, Uk. 350*)
- ❖ Kuzuru makaburi Ijumaa asubuhi baada ya Swalah ya Alfajiri inapendekezwa zaidi. (*Fatawa Razawiyyah, Juz 9, Uk 523*)
- ❖ Usizuru Makaburi usiku ukiwa peke yako.
(*Fatawa Razawiyyah, Juz 9, Uk 523*)
- ❖ Ni bora kuzuru makaburi katika usiku mtukufu, Haswa usiku wa Nisf Shaaban.
(*Fatawa 'Aalamgiri, Juz ya 5, Uk. 350*)
- ❖ Ni bora pia kuzuru makaburi siku tukufu kama vile siku za Eidi mbili (Eid-ul-Fitr na Eid-ul-Adha), siku ya kumi ya Muharram na siku kumi za mwanzo wa Zul-Hijjah. (*Ibid*)

Kufukiza Udi Juu Ya Kaburi

- ❖ Usifukize udi juu ya kaburi kwa kua hili ni kama kutoheshimu na halipendezi na maiti anaudhiwa nayo. Ikiwa mtu amekusudia harufu nzuri kwa wanaozuru basi atakiwa kufukiza udi mbali na kaburi, kwa kua kusambaza harufu nzuri ni kitendo kinachopendekezwa.

(Fatawa Razawiyyah, juz. 9, uk. 482)

Kuweka Mshumaa Juu Ya Kaburi

- ❖ Usiweke mshumaa uliowashwa juu ya kaburi. Kama huna tochi, simu ya mkono yenye tochi, na ikiwa hakuna taa zozote za barabarani za serikali au ikiwa zimezima, na unahitaji kuangaza ili utembe kwenye njia au kusoma Quran Tukufu katika giza la usiku basi waweza kuweka mshumaa au taa katika ardhi tupu upande mmoja wa kaburi, ikiwa ardhi hiyo tupu sio pale kulipokua na kaburi awali ambalo limeondolewa.
- ❖ A'la Hadrat رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ amenukuu: Imeelezewa katika kitabu cha *Sahih Muslim* kua wakati wa kifo chake Sayiduna 'Amr Bin 'Aas رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ alimlekeza mwanawe, 'Wakati nikifa sitaki mwanamke yeyote anayeomboleza aandamane na maiti yangu wala moto wowote.' *(Sahih Muslim, uk. . 75, Hadithi 192; Fatawa Razawiyyah, Juz 9, Uk. 482)*

Kaburi lisilojulikani kama ni la Muislamu au Asiyekua Muislamu

- ❖ Wakati hali ya kaburi haijulikani kama ni la Muislamu au asiyekua Muislamu, hairuhusiwi kulizuru au kusoma Fatiha hapo. Ni Sunnah kuzuru kaburi la Muislamu na ni Mustahab (inapendekezwa) kusoma Fatiha hapo, na ni Haramu kuzuru kaburi la Kafiri na ni Kufuru kumtumia Thawabu. (*Fatawa Razawiyyah, Juz. 9, Uk. 533*)
- ❖ Hakuna madhara katika kujiwekea mwenyewe Sanda tayari lakini haina maana kuchimba kaburi na kuliweka tayari mbeleni kwasababu mtu hajui atakufa wapi.

(*Fath-ul-Bari, Juz.3, Uk. 183*)

صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ

Mpatie mtu mwengine kijitabu hiki baada ya kukisoma

Vuna thawabu kwa kusambaza vijitabu vilivyochapishwa na Maktaba -tul -Madina na vipeperushi vyenye maua ya madani katika hafla za harusi, mazishi, jitimahi, ziara, zefe za Maulidi n.k. Fanya tabia ya kuweka vijitabu katika duka lako kuwazawadi wateja wako kwa nia ya kuvuna thawabu. Tuma angalau kijitabu kimoja au kipeperushi cha maua ya Madani kwa kila nyumba jirani ukisaidiwa na watoto au wauzaji wa magazeti, ili uzidisha juhudi ya kuwasilisha wito wa kuelekea katika haki na kupata thawabu kubwa.

الْعَمَلُ بِرَبِّ الْعَالَمِينَ وَالشُّكْرُ وَالشُّكْرُ عَنْ سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ اَلَا يَعْزُبُ عَنْكَ يَا اَللّٰهُ مِنَ الْعِبَادَةِ الرَّغْبَةُ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِیْمِ

Kwa ajili ya kuwa muislamu meha mungu
na mwenye kusimamisha sala

Pitisha usiku wako kwenye jitimai ya kuhuisha Sunna ya Daw at-e-islami inayofanyika kila siku ya Alkhamis Kuamkia ijuma a ndani ya mji wako kwa nia ya kutaka radhi za Allah ﷺ pa moja na nia zingine nzuri. Ili upate kujifunza sunna kuwa na kawaida ya kusafiri siku 3 katika Madani Qafilah pamoja na Wapenzi wa Mtume [حل المسائل الفقهية](#).

Fanya Fikr-e-Madina kwa kujaza kitabu cha Madani In'amat na ukipeleke kwa Zimmedar (msimamizi) wa eneo lako tarehe mosi ya kila mwezi wa Madani.

Lengo langu la Madani: Nitajitahidi kujirekebisha mwenyewe e na watu wa ulimwengu mzima [إِنْ شَاءَ اللّٰهُ عَزَّوَجَلَّ](#).

Kwa ajili ya kujirekebisha wenyewe tunatakiwa tuzifanyie kazi Madani In'amat na kwa ajili ya kuwarekebisha watu wa ulimwengu mzima tunatakiwa tusafiri katika Madani Qafilah.



Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagaran
Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan

UAN: +92 21 111 25 26 92 | Ext: 7213

Web: www.maktabatulmadinah.com | E-mail: feedback@maktabatulmadinah.com